

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 01 The Adventures of Mbott the Toad

Author: Ibrahima Ndiaye

**LEARNING BY EAR 2010**  
**SHALL I TELL YOU SOMETHING?**  
**AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE**

**EPISODE 01: „THE ADVENTURES OF MBOTT THE TOAD“**

**AUTHOR: IBRAHIMA NDIAYE**

**EDITORS: YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,  
NAÏMA GUIRA**

**TRANSLATION: NATALIE GLANVILLE-WALLIS**

**PROOFREADING: TONY DUNHAM**

**Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor**

**CHARACTERS:**

1. NARRATOR (male, about 40 years old)
2. MBOTT THE TOAD (male, about 20 years old)
3. SINDAKH THE GECKO (female, about 20 years old)
4. KAKATAR THE CHAMELEON (male, about 30 years old)

## **INTRO/ PRESENTER:**

Je, ni lini mara ya mwisho kusikiliza ngano za vichimbakazi? Jana usiku? Wiki mbili zilizopita au miaka? Leo msikilizaji tunakukaribisha katika mfululizo wa vipinidi vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako tukisimulia ngano za vichimbakazi katika mada “**Je nikudokezee?**”, hekaya kuhusu utamaduni wa Mwafrika katika kudumisha amani na maadili mema miongoni mwa jamii. Mara nyingi ngano huwa kama fumbo linaloashiria ukweli halisi wa matukio duniani, lakini kisha baadaye ngano hizi hutumiwa kuwatoa taka wengi masikioni. Kama ujuavyo, watu wanapoishi pamoja kwa amani na kutangamana, hupindukia kuwa na uwezo mkubwa wa kubuni nyenzo za kuboresha maendeleo. Na ngano tunayoizungumzia hii leo, inahusu mbinu muafaka za kubuni nyenzo za kukabiliana na mizozo kwa kusudi la kuleta maridhiano katika jamii.

Yaani vipi unaweza kukabiliana na hali ngumu maishani? Au vipi unavyoweza kukabiliana na ukosefu wa imani, wivu, uchoyo na ubinafsi katika jamii? Katika kila ngano au hadhithi, mtu hakosi kujifunza jambo moja au mawili ambayo yanaweza kumsaidia maishani. Hivyo basi endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi ili ujifunze kwanini Chura hupenda kuishi katika mazingira machafu. Ngano ya Chura kuhusu urafiki, imani na usaliti.

### **1. MUSIC (*play as background for the entire script*)**

*liegt vor: DALET: LbE: LbE\_Märchen\_Musik\_01\_überarbeitet*

### **2. NARRATOR:**

Zamani za kale, palitokea Chura kwa jina Mbott ambaye alikuwa rafiki mkubwa wa mjusu kafiri kwa jina Sindakh. Wawili hao walipendana na kuaminiana sana. Lakini siku moja wakati jua limewaka na joto jingi, ghafla Chura akamtembelea rafiki yake mjusu kafiri Sindakh. Sindakh alikuwa akijipumzisha chini ya mbuyu mkubwa.

### **3. MBOTT THE TOAD:**

“Salaam, habari za leo Dadangu! Naona wajipumzisha.”

**4. NARRATOR:**

Akauliza kwa unyeyekevu!

**5. SINDAKH THE GECKO**

“Ndiyo Kakangu, jua ni kali na tumboni hamna chochote...nahisi njaa sana!”

**6. NARRATOR:**

Akajibu Mjusi Kafiri, huku akionekana mchovu sana.

**7. MBOTT THE TOAD**

“Basi kwanini tusiandamane? Naenda kutafuta maembe! Natamani kula maembe sana.”

**8. NARRATOR:**

Kwa kweli Mjusi Kafiri hangesubiri tena mualiko huo.Maskini kwa jinsi alivyokuwa akihisi njaa akajikokota na kisha hao wakaandamana!

**9. SFX: *Sounds of gecko and toad in the grass***

## 10. NARRATOR:

Wakiwa njiani, walitania na kucheka. Mara ghafla, Chura akaona shamba la maembe yaliyoiva na kutamanisha. Wote wakaanza kudondokwa na mate!

## 11. SINDAKH THE GECKO:

“Oh, rafiki yangu, leo tutakula shibe yetu! Yalivyoiva maembe yale yananifanya nidondokwe na mate. Sasa tufanya haraka kuyatunda kabla ya mwenye shamba kutukuta. Mimi nitapanda na wewe utabaki hapa chini kuangalia tusije tukakutwa. Kama kuna hatari yoyote wewe koroma tu kama kunipa ishara.”

## 12. NARRATOR:

Na bila kupoteza wakati, mjusi akapanda na kuanza kutunda maembe na kula moja baada ya jingine na kumsahau kabisa rafiki yake aliyeko chini.

## 13. SINDAKH THE GECKO (*eating noisily*):

“Hmm...Hmmm”

## 14. NARRATOR:

Basi Mjusi aliendelea kufurahia utamu wa maembe huku akitupa koko chini, nusra moja limgonde rafiki yake. Ufidhuli huu ukamfanya Chura kutokwa subira.

## 15. MBOTT THE TOAD:

“Wewe! Sasa mbona umenisahau rafiki? Unatunda na kula peke yako na mie mwenzako ndiye niliyekuonyesha matunda haya. Nirushie moja na mimi tafadhali.”

## 16. NARRATOR:

Mbott aliendelea kumsihi rafiki yake kwa kulalama, hali iliyomkasirisha sana Mjusi.

## 17. SINDAKH THE GECKO:

“Hebu sikiliza hapa, wacha kulalama kama maskini wa kuomba omba barabarani. Lalama zako sasa zimeanza kunikera! Kwani mara ngapi nitakuambia kwamba mtu hapaswi kuzungumza akiwa na chakula mdomoni. Hufai kabisa kutembea na mimi au kuwa rafiki yangu.”

## 18. NARRATOR:

Mjusi akaendelea kufurahia mlo wake juu ya mwembe.

## 19. SINDAKH THE GECKO: *eating noisily*

## 20. NARRATOR:

Akiwa amegadhabishwa sana na tabia ya uchoyo wa Mjusi, Chura alifahamu kwamba ni kazi bure kuendelea kulalama.

## 21. MBOTT THE TOAD:

“Nakushukuru sana Dadangu! Ndio sasa nafahamu vyema kwanini Bibi yangu kwa busara zake kila mara alikuwa akiniusia kwamba hakuna tena uaminifu...lau ungekuwepo. Maji anamoishi Samaki, hayangetumika kumpika samaki huyo huyo?”

## 22. NARRATOR:

Kisha wazo likamjia Chura. Akawasha moto mkubwa chini ya mwembe. Kutokana na moshi uliokuwa ukifuka chini ya mwembe, Mjusi alianza kukohoa.

## 23. SINDAKH THE GECKO:

“Unafanya nini huko chini, kwani husikii joto? Au unachoma maembe? Wacha upuuzi wako Chura!”

## 24. NARRATOR:

Chura alimpuuzi tu. Mjusi aliendelea kukohoa kiasi cha kutapika maembe yote aliyoyabugia.

## 25. SINDAKH THE GECKO: *coughing fit*

## 26. NARRATOR:

Na baada ya kimya cha muda mrefu Chura akamjibu

## 27. MBOTT THE TOAD:

“Samahani sana rafiki Dadangu. Nimesikia baridi sana hapa chini, na kila mara ninapohisi baridi ya aina hii, mimi hupoteza hata sauti, hilo ndilo tatizo langu kubwa!”

## 28. NARRATOR:

Na kisha bila ya kuzungumza zaidi, Chura aliendelea kupepea ule moto hadi moshi ukatapakaa kote kwenye mwembe huo. Mjusi akateleza na kuangukia chini kwenye makaa ya moto. Japo alinusurika, majeraha aliyopata bado ni kumbukumbu. Ndio maana ukamuona mjisi na madoadoa kote mwilini mwake.

**29. SFX: *Free fall of the gecko***

**30. NARRATOR:**

Baadaye Mjusi alienda kumshtaki Chura kwa wanakijiji kwamba Chura huyo goigoi anamuonea wivu kutokana na uwezo na ujasiri wake wa kupanda miti. Na ndio sababu kubwa ya kumrushia makaa ya moto wakati amelala.

Hivyo wanakijiji wakatangaza msako dhidi ya Chura ili wamfunze adabu.

Mjusi alitafuta hifadhi katika nyumba ya Kinyonga Kakatar. Kakatar ni kongoti aliyeheshimiwa na wote katika jamii hiyo. Lakini baada ya kusimulia hadhithi yake, Chura akamuomba kitu kimoja tu.

**31. MBOTT THE TOAD:**

"Tafadhali nakuomba Kakatar nisaidie, mimi ni mdogo na mdhaifu sana. Siwezi kujilinda, tafadhali nakuomba unisaidie.

**32. NARRATOR:**

Kakatar alimpa dawa ya miujiza au uchawi na kumweleza :

**33. KAKATAR THE CHAMELEON:**

"Dawa hii ninayokupa, ni ishara ya nguvu. Unaweza kuinywa kwa masharti tu kwamba kamwe hutatumia vibaya nguvu zake!"

**34. MBOTT THE TOAD:**

"Nakuahidi nitafanya hivyo."

**35. NARRATOR:**

...Akasema Chura kwa unyenyekevu. Na bila ya kupoteza muda akanywa ile dawa na kuondoka nyumbani mwa Kinyonga .

**36. MBOTT THE TOAD: *drinks noisily***

**37. NARRATOR:**

Huku akijigamba, Chura alitaka kuwatawala wanyama wengine. Na akawakusanya wote isipokuwa Kinyonga Katarar na kutangaza:

**38. MBOTT THE TOAD:**

“Kuanzia leo nitamtawala na yule atakayethubutu kuhoji, nitapambana naye!”

**39. NARRATOR:**

Mkusanyiko wote huo ulimpuuzwa, hasa rafiki yake Mjusi aliyemcheka kwa kumkejeli.

Chura alimrukia Mbott na kumshambulia, nusra kumuua huku wanyama wengine wakitazama kwa hofu na mshangao.

Sungura mjanja Leuk, pia akajaribu kumkabili Chura, lakini pia yeye hakufaulu kwani alijikuta amerushwa na kuanguka katika shamba lililoko karibu. Hata Kifarur na Simba pia wakasalimu amri mbele ya Chura huyo. Katika hekaheka hizo, Ndovu akakasirika na kujaribu kumkabili Mbott huku akinguruma kama kawaida anapokasirika. Na kila mmoja akanyamaza kimya kwa hofu.

Chura alimrukia Ndovu kwenye sikio lake na kuanza kukoroma, hali iliyomkanganya kabisa Ndovu huyo akidhani kwamba ameanza kushikwa na wazimu. Ndovu alijaribu kumtoa Chura kwenye sikio kwa kutumia mkonga wake lakini pia hilo halikufua dafu. Akaanza kikumbia mzunguko akitapatapa, hali iliyowashangaza sana wanyama wengine.

#### **40. ELEPHANT: *Trumpeting and trampling***

##### **41. NARRATOR:**

Mshindo wake ulitingisa ardhi na hata kumuangusha Kinyonga Kakatar aliyekuwa amejituliza kwenye mti wake umbali wa kilomita kadhaa. Hivyo akafunga safari kwenda kujua chanzo cha mshindo huo wa kutisha. Na akastaajabu kuona mkusanyiko wa wanyama wote, huku Ndovu aliyekasirika akivuruga eneo hilo. Baada ya kufahamishwa kilichokuwa kikiendelea, Kinyonga Kakatar alitingisa kichwa kwa masikitiko.

##### **42. KAKATAR THE CHAMELEON:**

“Mbott! Umeshindwa kudumisha ahadi yako! Sasa kama adhabu kwako, nimekupokonya nguvu zote na kuanzia leo utakuwa ukiishi katika mazingira machafu zaidi ulimwenguni!”

##### **43. NARRATOR:**

Na bila ya kupoteza muda zaidi, alimshika Chura kwa kutumia ulimi wake na kumrusha mbali kabisa....

##### **44. SFX: “SPLASH” (*Sound of an object falling in a puddle of mud*)**

##### **45. NARRATOR:**

Mbott alianguka kisimani kwenye tope jingi ambako amekuwa akiishi hadi sasa.

*Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na atakayekuwa wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu..*

Learning by Ear 2010

Series: 'Shall I tell you something? African fables for a culture of peace'

Episode: 01 The Adventures of Mbott the Toad

Author: Ibrahima Ndiaye

## 45. Music

### **OUTRO/ PRESENTER:**

Msikilizaji tumefika mwisho wa ngano yetu kuhusu masaibu ya Chura. Ngano hii imeandikwa na Ibrahima Ndiaye kutoka Senegal, ambaye tunaamini kwamba Bibi yake alimuhadithia ngano nyingi za kuisimua ambazo utazisikia katika makala haya ya Noa Bongo! Jenga Maisha yako.

Je, nini maoni yako kuhusu hadithi hii? Au umewahi kujihisi na nguvu nyingi kupita kiasi? Tafadhali wasiliana nasi kupitia email yetu [lbe@dw-world.de](mailto:lbe@dw-world.de) au pia unaweza kusikiliza tena vipindi vya Noa Bongo kupitia mtandao wetu wa [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe). Na hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa!

END